

**Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”**  
“**Mizozo na utatuzi-Palipo na wazee**”  
Kipindi cha 4: “Mashujaa wasotambulika”  
Author: Chrispin Mwakideu  
Editor: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

## **List of characters by scene:**

### **SCENE ONE : SHANI AND LELA AT THEIR FARM**

- **Lela (f, 20)**
- **Shani (f, 17)**
- **Kavesi (m, 45)**

### **SCENE TWO : NINA, WOMEN AND CHILDREN AT WALIANI'S HUT**

- **Nina (f, 40)**
- **Waliani (m, 75)**
- **Pato (f, 35)**
- **Tubu (f, 35)**

### **SCENE THREE: TENSION AT THE RIVERSIDE**

- **Kavesi (m, 45)**
- **Masambo (m, 50)**
- **Mitumba (m, 50)**
- **Waliani (m, 75)**
- **several men for chanting (at least 6)**
- **several women (at least 4)**

## **Msimulizi**

### **INTRO:**

Salaam tele na karibuni katika kipindi chetu cha Noa bongo! Jenga maisha

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”

“Mizozo na utatuzi-Palipo na wazee”

Kipindi cha 4: “Mashujaa wasotambulika”

Author: Chrispin Mwakideu

Editor: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

yako. Hiki ni kipindi cha nne katika tamthilia yetu tukiangazia mizozo na utatuzi, kwa jina “ **Palipo na wazee**”. Katika kipindi kilichopita, ugomvi uliibuka kati ya Mitumba na Masambo, wanaume hawa wawili wanagombania rasilimali kwa ajili ya kuzikimu familia zao. Masambo aliiongoza mifugo yake shambani mwa Mitumba, baada ya Mitumba kuizua mifugo yake kunywa maji mtoni . Wote walilaumiana na kuungwa mikono na makabila yao. Kweli mzozo huu utapata utatuzi? Kama njia ipo, ni ipi? Endelea kusikiliza kipindi cha leo kiitwacho “**Mashujaa wasotambulika**”. Tunaanza pale Shani na Lela, walipopigwa na butwaa kuliona shamba lao lilivyo sambaratishwa.....

## **SCENE ONE: SHANI AND LELA AT THEIR FARM**

**1. SFX: HEAVY RAIN STARTS TO FALL / STORM.**

**2. SHANI:** **(Weeping and wailing)** Kwanini watutendee hivi!

Kwanini kutufanyia unyama kama huu!

**3. LELA:** Shani, kunanyesha. Turudi nyumbani.

**4. SHANI:** La! wacha mvua ininyeshee. Lela, tumefanya kazi ya bure! Kila mbegu tuliyopanda, muda tulitumia, nguvu zetu. Zote zimepotea! **(weeping)**

**5. LELA:** **(Breaking down in tears too)** Shani, utashikwa na homa. Turudi! Hata mimi nasikia vibaya pia, lakini hatuna la kufanya. Tumepoteza kila kitu.

**6. SHANI:** Siondoki! Nitaketi hapa mpaka baba atakaporudi.

**7. KAVESI:** **(Calls out)** Lela, Shani ..Mungu wangu! Shamba lenu limefanywa nini?

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”

“Mizozo na utatuzi-Palipo na wazee”

Kipindi cha 4: “Mashujaa wasotambulika”

Author: Chrispin Mwakideu

Editor: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

- 8. LELA:** Hatujui, lakini inaonekana ni kama mtu amekuja kulisha mifugo yake shambani mwetu! Kavesi, kwanini binadamu watendeane unyama kiasi hiki?
- 9. KAVESI:** (with rage) Ni wale waTorube! Lakini leo ni leo! Kwanza ninachelewa.
- 10. SHANI:** Unachelewa kufanya nini?
- 11. KAVESI:** Kwani baba yenu hakuwaeleza?
- 12. LELA:** Kutueleza nini? Kavesi, baba yetu yuko wapi? Tumemsubiri muda mrefu sana...
- 13. KAVESI:** Baba yenu na wote wa kabilia letu tumechoshwa na ukiritimba na uchokozia wa waTorube, Nina hakika ni Masambo aliyeharibu shamba lenu. Tulizuia ng'ombe zake zisinywe maji mtoni, naye akilipiza kisasi. Lakini leo atalipa na uhai wake!

#### **14. SFX: BRANDISHING A MACHETE OR CRUDE WEAPON**

- 15. SHANI:** Ndio kwa maana umebeba hiyo silaha ? ili mukapigane na waTorube?
- 16. KAVESI:** Ndio! Lazima mtu atalipia uovu huu. Leo ni mwisho wao! Wasichana, musiketi mvuani, nendeni nyumbani mutuombee sisi na baba yenu. Tuweze kurudi na ushindi!
- 17. SHANI:** Lela, na je baba asiporudi?
- 18. LELA:** Usifikirie hivyo. Njoo Shani. Tayari unatetemeka.

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”  
“Mizozo na utatuzi-Palipo na wazee”  
Kipindi cha 4: “Mashujaa wasotambulika”  
Author: Chrispin Mwakideu  
Editor: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

**(Shani shivers from the cold rain)**

**19. SHANI:** **(Speaks as she shivers)** Lazima tufanye  
kitu..Lazima.

**20. MSIMULIZI:** Wakati dada hao wawili walionyeshewa na kupigwa na baridi wakielekea nyumbani, wanaume wote wa makabila hayo mawili walikua wamekutana katikati ya bonde wakisimama mkabala huku wamegawanywa na mto, nyimbo za vita zikipaa hewani na kufedheheshana. Wakati huo, Nina alikua amekusanya wanawake wote wa kabilia lake, pamoja na watoto, na wakaenda kutafuta wasia kwa mkongwe wa kabilia lao, Waliani.

**SCENE TWO: NINA, WOMEN AND CHILDREN AT WALIANI'S HUT**

**21. SFX: SEVERAL BABIES CRYING**

**22. WALIANI:** Wanawake waTorube , ni nini kilichowaleta kwangu?  
Mimi sikumbukwi na yejote.

**23. NINA:** Tunahitaji msaada wako, Waliani. Wewe ndiye mzee zaidi kijijini kwetu. Bado unaheshimika, umetukuzwa, na miaka yako imekupa busara zaidi kutuliko sote.

**24. WALIANI:** Kuna shida gani? Naona jambo hili linahusu waume wenu. Kwa sababu sioni hata mmoja wao hapa.

**25. PATO:** Wote wameenda.

- 26. WALIANI:** **(surprised)** Yaani wamewaacha nyote?  
Wameendapi?
- 27. TUBU:** Wamekutana mtoni ili kuandaa vita na watu wa Koroma.
- 28. NINA:** Tumekujia msaada wako ili tupate suluhu, kabla damu ya waume wetu na vijana wetu ianze kumwagika mtoni.
- 29. WALIANI:** **(Thoughtful)** Hmm. Nilidhani kuna polisi, mahakama na mfumo wa haki uliowekwa na serikali. Mbona musiende huko kwa usaidizi?
- 30. NINA:** Hawatoelewa mkinzano huu kama unavyoolewa wewe, Waliani. Mbali na hayo, serikali pia inaweza kulemea upande mmoja. Tungelitaka mkinzano huu uishe na uamuzi wa haki. Pande zote mbili ziridhike, bila mmoja kuona dhuluma.
- 31. TUBU:** Muhimu zaidi kusiwe na hata kifo cha hata mtu mmoja.
- 32. PATO:** Suala la mahakama lahitaji pesa ambazo kwa sasa hatuna.
- 33. WALIANI:** Kuna njia moja ya kumaliza huu mkinzano. Wazee walitumia sana njia hii. Lakini itamuhusisha kila mtu. Ikifanywa sawasawa, italeta uponyaji na maridhiano.
- 34. NINA:** Tuko tayari! Tutafuata maagizo yako.
- 35. WALIANI:** Basi mtu ni lazima awafahamishe watu wote, wazee na wanawake kutoka kabilia la Koroma na wote wateremke mtoni na watoto wao..

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”  
“Mizozo na utatuzi-Palipo na wazee”  
Kipindi cha 4: “Mashujaa wasotambulika”  
Author: Chrispin Mwakideu  
Editor: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

- 36. TUBU:** Hata watoto wachanga?  
**37. WALIANI:** Nimesema wote. Hebu mtu anipe bakora yangu.

**38. SFX: SOMEONE USING WALKING STICK TO WALK**

**39. MSIMULIZI:** Mtumishi alitumwa na kueleza haja ya wakaazi wote wa bonde la Kijani kukutana mtoni kwa sherehe ya amani na maridhiano. Lakini, watafaulu? Hebu tuchunguzeni. Kwa sasa kule mtoni, tafrani limetanda, chuki, masimango na nyimbo za vita zinazidi kutokota...\_

**SCENE THREE: TENSION AT THE RIVERSIDE**

**40. SFX: RIVER RUNNING SMOOTHLY**

**41. (Group of men chanting and rumbling in preparation for war)**

**42. KAVESI:** (**close, shouting**) Wa Koroma! Nilipokuwa ninakuja , niliona jambo la kusikitisha sana. Lela na Shani, mabinti wa Mitumba, walikuwa wananyeshewa, wanalia na kujigaragaza mchangani kwenye ardhi ya baba yao. Maadui zetu wale walio upande wa pili wa mto, wamelisha mifugo yao shambani kwa Mitumba na kula mimea yote waliyopanda. Hivi ninavyozungumza hamna hata unyasi katika ardhi hiyo.

**43. MITUMBA:** (**close, in agony**) La! Haiwezekani! Masambo,

**Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”**

**“Mizozo na utatuzi-Palipo na wazee”**

Kipindi cha 4: “Mashujaa wasotambulika”

Author: Chrispin Mwakideu

Editor: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

umechukua uhai wangu leo! Hiyo si haki, lazima  
nichukuwe uhai wako!

**44. (MEN ANSWER IN CHANTS OF “YES! YES! YES!”)**

**45. MASAMBO:**     (distant, shouting) Nyinyi watu wa Koroma! Nyinyi  
ndio waanzilishi wa haya. Kwanza, mulivamia ardhi  
yetu.

**46. (MEN ANSWER SOME IN CHANTS OF “YES!” (DISTANT) SOME IN  
CHANTS OF “NO!” )**

**47. MASAMBO:**     (distant, shouting) hamukutosheka, mukaiba maji  
yanayotiririka kutoka kwenye huu mto, kupeleka  
kwenye mashamba yenu. Wanyama wetu watatoa  
wapi maji? Bibi na wototo wetu? Ulafi ni sharti ukome!  
Na ukome hivi sasa! (**Calls out**) Torube hei!!!!!!

**48. (Men answer in response, “hei!!!!!!”)**

**49. MASAMBO:**     (distant, shouting) Tuwamalizeni !

**50. MITUMBA:**     (close, shouting)) Jitayarisheni kuilinda ardhi yetu!

**51. SFX: Humming Song of peace led by Nina, Lela, and other women  
(approaching)**

**52. MASAMBO:**     (approaching, shocked) Nina! Unafanya nini hapa?  
Na kwanini umeandamana na wa Koroma?

**53. MITUMBA:**     (approaching, shocked too) Lela! Shani! Mbona  
mumeungana na maadui zetu?

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”

“Mizozo na utatuzi-Palipo na wazee”

Kipindi cha 4: “Mashujaa wasotambulika”

Author: Chrispin Mwakideu

Editor: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

**54. WALIANI:** **(close)** Hawa wanawake wana hekima kuwaliko.

Wanakunywa maji ya mtu huu mmoja ambao nyinyi  
munaupigania kama maadui, lakini wao wanataka  
amani na heri ya familia zao. Wana ..

**55. MASAMBO:** **(Disapproving)** Hawafai kuwa hapa! Huu si wakati  
na wala hapa si pahala pa watoto na wanawake!

**56. WALIANI:** **(Commanding)** Masambo nyamaza! Unawezaje  
kunikata kauli nikizungumza? Nyinyi watu mumeacha  
taratibu za babu zetu. Wakati wangu, hakuna mtu  
angelizungumza mbele ya mzee! Hiyo ni miko!

**57. MASAMBO:** Samahani, mzee Waliani. Tafadhali usamehe ujinga  
wangu na laana yako au hasira isinifike mimi wala  
kizazi changu.

**58. WALIANI:** Na iwe hivyo. Sasa najuwa kila mmoja wenu amebeba  
silaha anataka kuvamia mwengine. Lakini kabla ya  
hayo, nawarai kwa jina la mababa zetu, muipe amani  
na maridhiano nafasi... guu langu hapa ni kwa ajili ya  
amani.

#### **59. SFX: BABIES START TO CRY**

**60. WALIANI:** Hebu watazameni watoto wenu, bibi zenu, kisha  
mufikirie..huu unaweza kuwa ndio mwisho wenu nyinyi  
kuwaona. Tunaweza kusuluuhisha tofauti zetu hivi  
sasa, hapa tulipo, au tughairi. Tufutate njia ile ambayo

**Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”**

**“Mizozo na utatuzi-Palipo na wazee”**

Kipindi cha 4: “Mashujaa wasotambulika”

Author: Chrispin Mwakideu

Editor: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

nyinyi wenyewe tayari mumeshaichaguwa,  
itakayotuachia vilio, mayowe, wajane na yatima.

**61. MITUMBA:** Lakini Waliani, hii familia ya Masambo wameliharibu shamba langu lote. Nitawasamehe vipi mimi?

**62. MASAMBO:** Nilifanya hivyo baada ya mifugo yangu kuzuiliwa isinywe maji kutoka mtoni. Mto wetu!.

**63. WALIANI:** Naelewa uchungu ulionao Mitumba. Nimearifiwa kuwa Masambo pia alipoteza ng'ombe zake kwa wezi wa Kimbebe. Ndipo nikasema, kila mmoja ana chuki na mwenzake. Lakini ni lazima kumaliza hii chuki, uhasama, huu uovu. Sote ni sharti tujitolee. Hasa Mitumba na Masambo. Kwa kuanza shughuli hiyo. Nimekuja na jogoo.

#### **64. SFX: COCK MAKES SOUNDS**

**65. WALIANI:** Nawataka nyinyi wawili, Masambo na Mitumba, muje hapa nilipo, na museme yote yaliyo miyoni mwenu. Baada ya hapo tumchinje jogoo huyu, kisha tuiombe mizimu ituondolee chuki hiyo. Lakini kabla ya kufanya hivyo, naomba kila mwenye silaha aiweke chini.

#### **66. SFX: MEN MUMBLE. IRON SHAPED WEAPONS BEING PLACED DOWN**

**Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”**

**“Mizozo na utatuzi-Palipo na wazee”**

Kipindi cha 4: “Mashujaa wasotambulika”

Author: Chrispin Mwakideu

Editor: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

## **OUTRO:**

Waume wa pande zote mbili waliweka chini, mashoka, magongo, mikuki, nyuta na mishale ya sumu. Lakini upatanishi wa Waliani utafua dafu? Kwa hayo tunafikia mwisho wa kipindi chetu cha nne kiitwacho “ **Palipo na wazee**”. Jiunge nasi wiki ijayo ungundue ni yapi yaliyotendeka. Ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki au vyengine vilivyopita au kutuma maoni, tembelea tovuti yetu [www.dw.de/kiswahili](http://www.dw.de/kiswahili)

Mpaka tutakapokuwa wageni wako tena. Kwaheri.